*Kioo cha Lugha, Juz. 19(1), 2021, 145-160*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Euphrase Kezilahabi: Jabali katika Utetezi wa Uafrika

*Stella Faustine*[1]

## Ikisiri

Jina Euphrase Kezilahabi si geni katika ulimwengu wa fasihi. Umahiri katika uandishi wa kazi zake za fasihi, umezua mijadala mingi katika uga wa taaluma. Kimsingi, mijadala hiyo inabainisha mchango wake katika maendeleo ya fasihi, kwa namna kazi zake zinavyojipambanua kifani na kimaudhui. Hata hivyo, pamoja na mijadala ya wataalamu hao kuutajirisha uga wa kitaaluma kwa kujadili mchango wa nguli huyo katika maendeleo ya fasihi, bado suala la namna Kezilahabi anavyojipambanua katika kuutetea Uafrika, halijatazamwa kwa kina. Makala hii inaziba pengo hilo la kitaaluma kwa kubainisha namna mwandishi huyo alivyojipambanua katika kuutetea Uafrika, mahususi katika mwegamo wa kitamaduni. Data zilizozalisha makala hii zilikusanywa maktabani na uwandani. Data za msingi zilikusanywa kutoka katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo, Nagona,* na diwani ya *Karibu Ndani.* Data hizi zilipewa ithibati na data za upili zinazohusiana na mada husika ambazo zilikusanywa uwandani na maktabani. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulifanyika kwa kutumia Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Makala imebainisha namna Euphrase Kezilahabi anavyojipambanua katika kuutetea Uafrika kupitia maisha yake halisi na katika kazi zake za fasihi.

[1] Mhadhiri, Idara ya Kiswahili, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania. Baruapepe: stelafau@gmail.com

## 1.0 Utangulizi

Katika ulimwengu wa fasihi ni nadra sana kuwataja watu wenye mchango mkubwa katika ukuaji na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili pasipo kumtaja Euphrase Kezilahabi (1944 - 2020). Nguli huyu ameandika kazi mbalimbali za fasihi: riwaya, ushairi, tamthiliya na hadithi fupi ambazo kwazo, umahiri wake katika kuifungamanisha fani na maudhui ndio unaompa sifa zaidi. Miongoni mwa kazi zake ni riwaya ya *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka* (1979), *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Kazi za ushairi ni *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008). Pia, ameandika tamthiliya inayoitwa *Kaptula la Marx* (1999). Kwa upande wa hadithi fupi, Kezilahabi ameandika *Wasubiri Kifo* (1976), *Mayai - Waziri wa Maradhi* (1978), *Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani* (1985), *Magwanda Kubilya na Vyama Vingi* (1993), *Ulingo wa Uchaguzi* (1994) na *Balenzi* (2009). Kwa mujibu wa Gaudioso (2020) nguli huyu amewahi kuandika shairi mojamoja katika majarida na magazeti kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Nayo ni *The Nile* (1968), *Rock in Lake* (1969), *The Bulls Fight* (1969), *The Wind of Time* (1969) na *The Sad Virgin* (1969). Mengine ni *Kumbukumbu na Dhamiri Yangu* (1970) na *Kisu Mkononi* (1971). Baadaye, mashairi haya yalichapwa katika diwani ya *Kichomi*. Mengine ni *Mpiga Zeze* (1981) lililochapwa katika diwani ya *Dhifa* (2008) pamoja na *Kisima*, *Moshi Ukizidi Pangoni*, *Kifo cha Mende Wekundu* na *Ngoma ya Kimya* (2007*)* ambayo yalichapwa katika diwani ya *Karibu Ndani*. Mawanda haya ya kiuandishi, yamesababisha wataalamu mbalimbali kumpa sifa kadhaa. Kwa mfano, Senkoro (1995) anaonesha umahiri wake kwa kumfananisha na Shaaban Robert. Pia, Chuachua (2011) anathibitisha umahiri wa nguli huyu kwa kusema:

> Euphrase Kezilahabi ni athura wa Shaaban Robert… Ni miongoni mwa waandishi nguli wa Fasihi. Unguli huu anaupata wakati maandishi yake yamebeba vipengele kadhaa toka katika maandishi ya Shaaban Robert (uk. 158).

Umahiri wa kazi za Kezilahabi kama anavyoeleza Chuachua (*khj*), umevuta nadhari kubwa na kuzua mijadala mingi miongoni mwa watafiti wa kazi za fasihi. Faustine (2017) anabainisha hili kwa kusema kuwa, mijadala hiyo imetokana na namna mwandishi anavyovifungamanisha vipengele vya fani na maudhui katika kuwasilisha ujumbe wake. Mulokozi (1988) anaeleza uhusiano kati ya mtu binafsi na jamii. Kwa kutumia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, anabainisha namna idili za jamii zinavyomfunga mtu binafsi kufanya fujo zake ingawaje hiari ya kufanya fujo hizo imekitwa katika matakwa binafsi. Kimsingi, andiko hili linatoa mtazamo wa jumla kwa jamii kuwa uhuru wa mwanadamu umefungwa katika misingi ya kimaadili ya jamii husika.

Musau (1985) kupitia riwaya za *Rosa Mistika*, *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* ameshughulika na suala la maana ya maisha kama linavyosawiriwa na Kezilahabi. Kwa mujibu wa mtafiti huyu, kazi hizo ni tafsiri ya hali halisi ya maisha ya Kezilahabi inayomwonesha kama mtu aliyekata tamaa kwa kuwa duniani ni mahala ambapo hakuna furaha. Utafiti huu unadhihirisha bayana kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi anapoandika kazi yake, yale anayoyaandika hayatoki katika ombwe bali ni akisio la mazingira yanayomzunguka.

Mbatiah (1988) anabainisha mabadiliko ya uandishi wa Kezilahabi kutoka kipindi cha uhalisia mpaka kipindi cha riwaya za kimajaribio. Anafafanua kuwa riwaya za kimajaribio zilizoandikwa na Kezilahabi zinaonesha wazi kushindwa kwake kiuandishi kwani hazieleweki kwa jamii. Suala hili linapingwa na Faustine (2012) kwa kusema kuwa kama msomaji haelewi kazi husika ya fasihi, basi huyo siyo hadhira kusudiwa ya mwandishi. Suala la mabadiliko katika uandishi wa Kezilahabi linajadiliwa pia na Khamis (2007). Khamis, kwa kurejelea riwaya ya *Nagona*, anaonesha mabadiliko ya usawiri wa wahusika na kubainisha kuwa Mimi ni mhusika asiye na nyama wala mifupa bali ni kivuli tu kinachobainisha mawazo ya mwandishi. Mabadiliko ya uandishi wa kazi za fasihi za Kezilahabi kama yanavyofafanuliwa na Mbatiah (*khj*) na Khamis (*khj*), hayabainishi tu kiwango cha ukuaji wa mwandishi kisanaa bali hudhihirisha pia ni kwa namna gani mabadiliko ya jamii yanavyoweza kuathiri mabadiliko ya kazi za fasihi.

Watafiti wengine ni Wamitila (1999) na Senkoro (2006) ambao wameeleza maana ya majina kwa namna yanavyotumiwa na Kezilahabi katika kazi zake. Wamitila (*khj*) anaona kuwa majina mengi anayoyatumia yametokana na mazingira halisi ya jamii ya Kikerewe ambako ndiko alikozaliwa Kezilahabi. Nao, Chuachua (2016) na Faustine (2017) wameonesha ni kwa namna gani kazi za Kezilahabi ni akisio la maisha halisi ya Mwafrika kwa kubainisha namna kazi hizo zinavyoakisi mitazamo ya kifalsafa ya Waafrika. Chuachua (*ktj*) amejadili namna epistemolojia ya Wabantu inavyojibainisha katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Nagona* na *Mzingile*. Faustine (*ktj*) ameangalia ni kwa namna gani falsafa ya Kiafrika inachangia kujenga mtindo wa uhalisiajabu. Miongoni mwa kazi alizotumia katika utafiti wake ni *Nagona* na *Mzingile*. Kimsingi, watafiti tajwa hapo juu hawajabainisha namna Kezilahabi anavyoutetea Uafrika katika kazi zake za fasihi. Hivyo basi, makala hii inapanua mawanda ya kimtazamo kwa kuangalia ni namna gani Kezilahabi anautetea Uafrika katika mtazamo jumuifu kifani na kimaudhui na siyo kwa kujikita katika kipengele cha kifalsafa peke yake.

Pamoja na tafiti hizo kubainisha umuhimu mkubwa na mchango wa Euphrase Kezilahabi katika uga wa kitaaluma mahususi fasihi ya Kiswahili, bado kuna mwanya mkubwa wa kimaarifa katika kubainisha ni kwa namna gani nguli huyu amejipambanua katika kuutetea Uafrika, katika maisha yake halisi na ndani ya kazi za fasihi.

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti

Usanifu wa utafiti huu ni wa kifenomenolojia. Huu ni usanifu ambao hutumia sayansi katika kutafuta ukweli wa jambo fulani kwa mtu mwenye ujuzi au uzoefu wa jambo hilo kwa kuhusisha na uhalisi wa maisha (Ponera, 2019). Data zilikusanywa maktabani na uwandani kwa kutumia usampulishaji usio bahatishi. Kwa upande wa maktabani, makala, vitabu na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na mada husika zilifanyiwa mapitio. Vitabu vya riwaya vya *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Nagona* na diwani ya *Karibu Ndani* vilitumiwa kupata data za msingi. Hivi vilipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa wa kipekee kutokana na kuwa na maudhui yanayolandana na malengo ya utafiti. Uwandani, makundi mawili ya watoataarifa yalisailiwa. Kundi la kwanza ni la wanafunzi wanne (4) wa Kezilahabi ambao pia ni watafiti katika fasihi ya Kiswahili. Kundi la pili ni ndugu wa karibu watatu (3) wa Kezilahabi kutoka wilayani Ukerewe alikozaliwa. Makundi yote mawili yalipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa tajwa ambapo mtoataarifa aliyekwishasailiwa hupewa nafasi ya kumpendekeza mtu mwingine mwenye sifa zinazohitajika. Kwa jumla, makundi yote mawili yanasadikiwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na kazi za Kezilahabi, na pia uelewa wa karibu kuhusu maisha yake nje ya uandishi. Data zilizopatikana zilipangwa kulingana na maudhui husika. Data hizo zilichanganuliwa, kufafanuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

## 3.0 Mwega wa Uchambuzi na Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Mwasisi wa nadharia hii ni mwanafalsafa Mfaransa aliyejulikana kwa jina la Hippolyte Adolphe Taine. Welleck na Warren (1949) wanaeleza kuwa Taine ndiye mtu wa kwanza kujadili uhusiano uliopo kati ya mtu na jamii kwa kutumia kanuni ya uchanganuzi wa jamii, mazingira na wakati. Akibainisha mawazo ya Taine, Chalmers (1973) anasema kuwa kazi ya sanaa huamuliwa na muktadha wa mazingira ya jamii. Hivyo, haina budi kuangaliwa kama ni taswira ya kijiografia, kiutamaduni na kimazingira iliyochimbuka kutoka katika jamii husika. Katika makala hii, Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi imetumika katika ukusanyaji, uchanganuzi wa data na uwasilishwaji wa matokeo kwa kuzingatia misingi mikuu miwili: Kwanza, ni ufungamanifu wa kazi za fasihi na yale yanayojitokeza katika jamii. Pili, kazi ya fasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira na kiutamaduni ambayo kazi hiyo imechimbuka kwayo. Hivyo, kwa kuzingatia msingi wa kwanza na wa pili wa nadharia, katika makala hii kazi teule zilizotumiwa zilitazamwa kama ni taswira za kitamaduni na kijiografia zinazoakisi maisha halisi ya jamii ya Waafrika.

## 4.0 Euphrase Kezilahabi na Uafrika

Katika kuutetea Uafrika, Kezilahabi amejipambanua katika namna mbalimbali. Namna ya kwanza ni kupitia maisha yake halisi ambapo anausemea Uafrika katika miktadha mbalimbali. Namna ya pili ni katika kazi zake za fasihi, ambapo amekuwa

na mchango mkubwa katika kuiendeleza fasihi ya Kiafrika kupitia maandishi yake. Makala hii inabainisha hilo kama inavyofafanuliwa katika mjadala ufuatao:

### 4.1 Matumizi ya Lugha za Kiafrika

Euphrase Kezilahabi amekuwa kinara wa kuutetea Uafrika kwa namna alivyojibidisha katika uhamasishaji wa matumizi ya lugha inayoeleweka kwa Waafrika katika nyanja mbalimbali. Utetezi wake unabainishwa kupitia maandiko yake yanayowataka waandishi wa kazi za fasihi kutumia lugha za Kiafrika, zinazoeleweka kwa hadhira pana ya Waafrika. Kezilahabi, anatoa ufafanuzi wake kuhusu umuhimu wa kutumia lugha za Kiafrika pale anaposema:

> Lakini leo … hapana haja ya mwandishi wa Kiswahili kujitetea. Mwandishi wa Kiswahili hana haja tena ya kujibu swali kama: kwa nini ulikata shauri kuandika riwaya zako katika Kiswahili? Swali hili nimeulizwa mara nyingi. Siku hizi silijibu. Hali ilivyo sasa Afrika Mashariki mwandishi anayepaswa kuwekwa jukwaani kujibu maswali ya umma ni yule anayeandika katika lugha ya wale wanaomtawala, hapa Tanzania ni lugha ya Kiingereza (Kezilahabi, 2003b: 226).

Nukuu hii inabainisha wazi dhamira ya Kezilahabi katika utetezi wa utamaduni wa Mwafrika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Mwandishi huyu hakuishia tu katika nadharia bali, pia katika utendaji ambao unajidhihirisha kupitia uandishi wa kazi zake za riwaya, ushairi, tamthiliya na hadithi fupi ambazo zimeandikwa kwa kutumia lugha fasaha ya Kiswahili. Kazi hizo ni zile ambazo zimeorodheshwa katika kipengele naamba 1.0.

Pia, jitihada za Kezilahabi katika kuutetea Uafrika zinajibainisha pale alipopinga kuandika tasnifu yake ya Umahiri kwa lugha ya Kiingereza. Jambo hili linaelezwa na Mutembei (2021)[2]:

> Harakati za Kezilahabi katika kuutetea Uafrika zilianza kuonekana mapema katika kazi zake za fasihi. Alikuwa mstari wa mbele katika uandishi wa kazi hizo kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kimsingi, hili ni jambo jema kwa Waafrika kwani alibainisha wazi kuwa tunayo lugha yetu kama Waafrika na inaweza kuwasilisha masuala mbalimbali katika maandishi kama zilivyo lugha nyingine. Pia, aliendelea kuutetea Uafrika wake mnamo mwaka 1976, kwa kukataa kuandika tasnifu yake ya umahiri kwa Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Alitetea hadi kukubaliwa kuiandika kwa Kiswahili.

[2] Prof. Aldin Mutembei ni mtaalamu na mtafiti wa Fasihi ya Kiswahili kutoka Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mahojiano yalifanyika kwa njia ya simu tarehe 15/03/2021.

Uamuzi huu wa Kezilahabi ulikuwa ni hatua kubwa ya jitihada zake, siyo tu katika kuutetea Uafrika, bali pia kuleta hadhi ya lugha na fasihi ya Kiswahili. Naye Euphrase (2021)[3] anafafanua zaidi namna Kezilahabi alivyopenda matumizi ya lugha za Kiafrika kiasi cha kuwafunza wanawe kwa kusema:

> Baba hakuwa mtu anayependa kujikweza. Alipendelea sana matumizi ya lugha za Kiafrika. Hii inadhihirika hata kupitia uandishi wa vitabu vyake mbalimbali ambavyo ameandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Alitupa uhuru wa kuchagua tunachokitaka lakini pia hakusita kuturudisha katika asili yetu. Tuliongea Kiswahili na alitufunza pia kuongea lugha za asili. Wakati wa likizo alipenda sana kutupeleka kutembelea kijijini Namagondo na pia Geita Sungusila kwa wazazi wake mama. Huko tulikutana na ndugu ambao walitufunza lugha.

Kwa jumla, dondoo hili linadhihirisha mapenzi ya dhati ya Kezilahabi katika kuthamini lugha za asili za Waafrika kama sehemu ya utamaduni wake. Hata hivyo, Euphrase (*khj*) ameendelea kubainisha wazi kuwa ingawa alisimama katika misingi ya Uafrika na kuutetea, mwandishi huyu aliamini pia katika uhuru wa mtu wa kuchagua kile anachoona kinamfaa zaidi.

Pia, ujasiri wa Kezilahabi katika kusimamia matumizi ya lugha za Kiafrika unadhihirika pale alipoamua kuwasilisha kazi yake ya Kiswahili ya *Rosa Mistika* (1971) katika shindano la kumtafuta mwandishi mzuri wa riwaya katika lugha ya Kiingereza. Gaudioso (2020) anaeleza kuwa wakati wa mahojiano baina yake na Kezilahabi, alipomuuliza ni kwa nini aliamua kuwasilisha riwaya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili katika shindano la riwaya zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza, alijibu kuwa ilikuwa ni kuwachokoza waandaaji. Hata hivyo, ingawa riwaya hiyo haikukidhi vigezo vya shindano kutokana na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili, ilionekana kuwa ni riwaya bora na kamati ya mashindano iliamua kuichapisha. Uamuzi wa Kezilahabi kuwasilisha riwaya hiyo katika shindano hilo, unatazamwa kuwa ni hatua kubwa katika kuitangaza na kuitetea fasihi ya Kiafrika.

### 4.2 Fasihi ya Kiswahili yenye Sura ya Uafrika

Miongoni mwa tunu anazopaswa kutunukiwa Kezilahabi ni zile zinazotokana na utetezi wake wa fasihi ya Kiswahili yenye sura na hadhi ya Kiafrika. Katika mijadala na kazi zake za fasihi, anaipambanua fasihi ya Kiafrika kifani na kimaudhui kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Fani ya Fasihi ya Kiafrika

Katika kipindi cha miaka ya 1970, ambacho wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili walitaka kujua ni nini hasa maana ya fasihi ya Kiswahili, Kezilahabi alijipambanua katika kubainisha misingi ya ushairi wa Kiswahili kifani. Kezilahabi

[3] Neema Euphrase ni binti pekee wa Prof. E. Kezilahabi. Mahojiano yalifanyika kwa njia ya simu tarehe 18/03/2021.

(2003a) anafafanua kuwa ushairi wa Kiswahili asilia haujibainishi katika umbo la vina na mizani bali hukitwa katika maana iliyokusudiwa. Kwa mtazamo wake, msisitizo unaowekwa katika utunzi unaozingatia vina na mizani kama uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili, humfanya mtunzi kuwa mtumwa na kusababisha uozo katika ushairi wa Kiswahili. Anasema:

> (Katika kuchunguza ushairi wa Kiswahili) kwanza kabisa (wachunguzi hao) hawakufikiri sana fasihi simulizi ambayo haikuwa katika umbo la vina na mizani. Mwanzo walikimbilia fasihi ambayo tayari ilikuwa imeandikwa. Zaidi ya hayo, hawakufikiri kabisa fasihi simulizi ya makabila yaliyokuwa karibu na Waswahili (uk. 153).

Kezilahabi anaweka wazi msisitizo wake wa kuwataka watunzi kurejea katika asili yao na sio kushikilia uzi wa urari wa vina na mizani ambao unawanyima uhuru wa kueleza mambo kwa mapana. Anazidi kufafanua kuwa kanuni hizo zinashikiliwa na wataalamu ambao hawakufanya uchunguzi wa kutosha kuhusu asili ya ushairi wa Kiswahili ambayo ni nyimbo za jadi zisizokuwa na urari wa vina na mizani. Msimamo huu wa Kezilahabi, unafafanuliwa zaidi na Mulokozi (2021)[4] pale anaposema:

> Kezilahabi amekuwa na athari kubwa katika ushairi wa kisasa. Kipindi cha mgogoro wa ushairi alitazamwa kama ni muasi wa ushairi wa Kiswahili. Alishikilia msimamo wake kwani hakuwa muumini wa mashairi yaliyokuwa yanaitwa mashairi jadi. Hii ni kwa sababu aliamini kuwa, urari wa vina na mizani si asili ya ushairi wa Kiswahili. Kwake aliona vitu hivi kama ni mapambo tu. Mara nyingi alirejelea nyimbo za ngoma, jando na unyago na za makabila mbalimbali na kuamini kuwa hizo ndizo chimbuko halisi la ushairi wa Kiswahili. Athari za mtazamo wake zilituathiri hata sisi wanafunzi wake tukaanza kutunga mashairi ya kisasa. Jambo hili lilizua mjadala mkubwa baina ya wanaushairi huru na wale wa kimapokeo.

Msimamo wa Kezilahabi kuhusu ushairi wa Kiswahili haukuishia tu katika malumbano ya hoja. Alitunga mashairi mbalimbali yasiyofuata urari wa vina na mizani kama mwongozo kwa watunzi chipukizi kutunga mashairi yao. Katika diwani yake ya *Karibu Ndani* (1988) anawakaribisha watunzi kutunga mashairi kwa

---

[4] Prof. Mugyabuso M. Mulokozi, mwanafunzi wa Prof. Kezilahabi, ni mtaalamu na mtafiti wa fasihi ya Kiswahili katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mahojiano yalifanyika tarehe 15/03/2021.

kuendana na utunzi wa fasihi uliofuata misingi na jadi ya nyimbo za makabila ya Kiafrika. Katika shairi la "Karibu Ndani", anasema:

1

Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lala salama
Katika mionzi hafifu, ya jua machweoni
Na mahadhi yagaagaa, juu ya bahari ya utenzi
Yameshindwa chini kuzama, kwenye kina cha urazini
Nao wahenga vibandani, nje tena hawatoki
Hakuna tena ngoma, ya kugeeana kani
Na ushairi umehama, umerudi upeponi
Lakini majani makavu, sasa hayatingishiki
Nayo madirisha ya nyumba, imara yamefungwa
Waliomo ndani wahofu hasira ya mizimu.

Muda si mrefu, patakuwa kiza totoro
Na wanyama wa usiku watazitawala taswira
Kwa kuwa njia naikumbuka msitu nitauingiya
Kwenye kiza cha karne. nyimbo mpya tatongoa
Tatumia silika ya uzawa, kuupata mwelekeo
Maana ushanga wa shingoni, bado sijautupa.

Katika sehemu ya kwanza ya shairi, mwandishi anaikaribisha hadhira yake katika utunzi wa ushairi huru. Hata hivyo, mshairi haoneshi tu namna ya utunzi wa ushairi huru bali anairejesha hadhira katika misingi ya utunzi wa Kiafrika pale anaposema: "Kwa kuwa njia anaikumbuka, msituni ataingia" akiwa na maana kuwa utunzi usiofuata urari wa vina na mizani si mgeni na ni wa asili, hivyo, anaukumbuka na ataingia katika dimba la washairi kutunga kwa kufuata misingi hiyo. Pia, anabainisha asili hiyo ya utunzi kuwa imetokana na misingi ya utunzi wa Kiafrika pale anaposema: "Tatumia silka ya uzawa, kupata mwelekeo" kwa maana kuwa anarejea na kuifufua misingi ya utunzi inayotokana na nyimbo za makabila ya Kiafrika isiyofuata urari wa vina na mizani kutunga kazi zake. Ni katika ukiushi huu ambapo Roberto (2021)[5] anafafanua kwa kusema:

> Kezilahabi hakuwa mtu wa Uafrika sana. Alipenda uhuru. Alitaka mtu achague kile alichoona kinafaa. Hakuwa mtu wa kuukumbatia Uafrika na kusema vingine havifai. Kezilahabi alikuwa ni mtu anayetafuta uhuru wa kuyawasilisha mawazo yake. Alikiuka misingi jadi ya utunzi wa mashairi ili aweze kuwa huru kuwasilisha mawazo yake katika fani anayoona kwake inamwezesha kuwasilisha mawazo hayo kwa urahisi.

[5] Roberto Gaudioso ni mwanafunzi wa Prof. Kezilahabi. Mtaalamu na mtafiti wa fasihi ya Kiswahili kutoka Napoli, Italia. Maoni haya yalitolewa katika Kongamano la Kumbukizi ya Prof. E. Kezilahabi tarehe 14/04/2021, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nukuu ya Roberto (*khj*) inatuongezea wazo la msingi kuhusu mitazamo ya Kezilahabi. Anaeleza kuwa Kezilahabi alikuwa ni mtu anayependa mtu achague anachoona kwake ni sahihi na siyo kung'ang'ania katika Uafrika. Hata hivyo, pamoja na maoni haya, bado hoja ya msingi inabaki katika mwelekeo wa mada yetu ya msingi kuwa ni kwa namna gani aliutetea Uafrika. Ieleweke kuwa, kusimamia misingi ya jambo fulani katika misingi ya kulitetea, haimaanishi kuwa unapingana na mambo mengine. Makala hii inabainisha wazi kuwa, ni katika kutetea kile anachoona kinafaa ndimo Kezilahabi alimopata uhuru wa kuyawasilisha mawazo yake.

Fani ya Kiafrika katika kazi za Kezilahabi inajitokeza pia kwa namna anavyowajenga wahusika wake wenye kusawiri mila na desturi za Waafrika. Kezilahabi (2003b) anathibitisha hili pale anapofafanua kuhusu uzuri wa kuwasawiri wahusika katika mazingira atokayo mwandishi kwa kusema:

> Ukitazama kwa uangalifu maandishi ya Kiswahili, waandishi ambao wamefanikiwa ni wale ambao wameweka wahusika hao chini ya misingi ya mazingira wanayoyaelewa na hasa yale ya kabila lao… Mimi mwenyewe niandikapo riwaya zangu nahakikisha kuwa wahusika wangu wanakulia na kukomaa Ukerewe Kisiwani na baada ya hapo ninaweza kuwafanya watembee na kukaa mijini Tanzania nzima (uk. 230-231).

Kezilahabi aliamini kuwa fasihi ya Kiafrika, lazima iendane na mazingira halisi ya Waafrika kuanzia ujenzi wa fani na maudhui. Hii inadhihirika katika riwaya zake ambapo anawajenga wahusika na mandhari zinazoakisi mazingira ya jamii za Waafrika. Jambo hili linafafanuliwa na Mbiti (2011) kuwa, Waafrika wana namna yao ya ugawaji majina ambayo huzingatia matukio yanayojitokeza katika jamii. Majina hayo huwa na maana zinazobeba uhalisi wa matukio hayo. Kwa mfano, katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, Kezilahabi anawajenga wahusika wake kwa kuwapa majina mbalimbali yenye asili ya kabila la Kikerewe yanayozingatia matukio ndani ya jamii hiyo. Miongoni mwa majina hayo ni Mungere, Kasala na Bugolola. Akifafanua kuhusu majina haya, Pantaleo (2021)[6] anaeleza:

> Kezilahabi alipenda sana kutumia majina ya mazingira ya nyumbani Ukerewe. Sisi tunapenda kupeana majina ya kurithi ambayo wakati mwingine yanatokana na tukio la wakati uliozaliwa. Kwa mfano, jina lake yeye mwenyewe Kezilahabi lina maana ya mtu aliyekuja wakati mbaya. Wakati anazaliwa kulikuwa na msiba nyumbani, hivyo, jina lake linaakisi mazingira hayo. Kwenye kitabu chake *Dunia Uwanja wa Fujo* kuna majina kama Mungere ambalo linatokana na samaki aina ya ngere. Mtoto wa kike

[6] Veneranda Pantaleo Muya ni mpwa wa Euphrase Kezilahabi. Anaishi Ukerewe Namagondo. Mahojiano yamefanyika kwa njia ya simu tarehe 29/03/2021.

> anapozaliwa kipindi cha mavuno mengi ya samaki hawa hupewa jina la Mungere. Bugolola linalotokana na neno la Kikerewe *kugolola* lenye maana ya kunyoosha. Hili mtu hupewa kutokana na matarajio ya wazazi kuwa huenda mtoto huyo amezaliwa na ndiye atakayeyanyoosha mambo katika familia yake. Hata hivyo, Ukerewe kuna makabila mengi. Majina mengine yametokana na jamii nyingine kama Wajita. Kwa mfano, jina Kasala ni jina lenye asili ya kabila la wajita lakini kutokana na mwingiliano wa kimahusiano hujitokza pia kwa Wakerewe.

Kwa upande wa riwaya ya *Nagona*, mwandishi ametumia jina Nagona ambalo kwa mujibu wa Bitende (2012) linafungamana na historia na muktadha wa maisha ya mtunzi. Ni jina la dada yake Kezilahabi, mtoto wa baba mdogo, aliyeishi kwa muda mrefu pasipo kupata mtoto. Baadaye, baba huyo alifanikiwa kupata mtoto wa kike na kumpa jina hilo akimaanisha kuwa mtoto huyo amekuja kumaliza matatizo aliyokuwa akiyapata katika jamii kutokana na tatizo lake la kutopata mtoto.

Maelezo haya yanajenga hoja kuwa Wakerewe kama jamii nyingine za Kiafrika hutoa majina yao kulingana na muktadha na mazingira aliyozaliwa mtoto. Matumizi ya majina haya katika kazi za Kezilahabi, yanapanua mawanda mapana ya kuutangaza utamaduni wa Waafrika kuhusu suala la utoaji majina, kueleza utamaduni wa Mwafrika; na pia, kukuza na kuthamini fahari ya Mwafrika.

### 4.2.2 Maudhui Yanayoakisi Maisha ya Waafrika

Suala jingine linalompambanua Kezilahabi kama mtetezi wa Uafrika ni namna anavyoyajenga maudhui yake yanayosawiri maisha halisi ya Waafrika katika kazi zake. Katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, anabainisha wazi taratibu za mahusiano ya ndoa kama sehemu ya kujenga utamaduni wa Waafrika. Anaeleza kuwa sifa kuu ya thamani ya ndoa ni kupata mtoto (Tempels, 1959; Mbiti, 2011; Faustine, 2017 na 2019). Hivyo, kipimo cha mwanamume kuhusu uwezo wake wa kupata mtoto ni urijali wake. Kezilahabi anaonesha hili kupitia mhusika Kapinga ambaye anashindwa kushiriki tendo la ndoa na mkewe siku ya ndoa. Kutokana na mila na desturi za jamii nyingi za Waafrika, ndoa hii inakuwa haina uhalali na hivyo humlazimu mke kurudi kwao (uk. 10).

Pia, anafafanua umuhimu wa mtoto kama mrithi wa baadaye kwa kadiri ya mitazamo ya Waafrika (Tempels, 1959; Mbiti, 2011 na Faustine, 2017). Katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, Kezilahabi anafafanua hili pale anaposema, “Kapinga alifurahi sana, alipata kijana mwanamume wa kurithi mali zake” (uk. 11). Anaendelea kubainisha hili katika *Nagona*, kwa kuonesha mtazamo wa Waafrika kuhusu umuhimu wa mtoto kama kiongozi wa familia. Hii inajitokeza pale anapoeleza matumaini ya kuzaliwa kwa Nagona. Huyu anatazamwa kama tumaini na muongoza njia, baada ya Mimi kushindwa kufikia matarajio ya kuikamilisha safari. Anasema:

> “Umejitahidi”, alisema. “Sina manung’uniko. Umeshindwa lakini katika kushindwa kuna ushindi. Kushindwa kwako kumeandaa njia ya majilio ya

> pili. Anaweza sasa kuzaliwa. Bado tunao mshale mmoja katika uta, wa kwanza umepotea (uk. 69).

Dhana ya ‘bado tuna mshale mmoja katika uta’, inaakisi mtazamo mpana wa falsafa ya Waafrika kuwa kuzaa watoto wengi ni baraka kwani hujui kesho ni nani atakayekusaidia (Faustine, 2017). Hii inamaanisha kuwa ijapokuwa mtoto wa kwanza hakufikia matarajio yaliyokusudiwa, bado kuna matumaini kwani kuna mtoto mwingine anayeweza kuongoza njia na kuyafikia mafanikio yaliyotarajiwa.

Kezilahabi ameongelea pia suala la maadili yanayokitwa katika misingi ya Kiafrika. Katika *Dunia Uwanja wa Fujo* anabainisha kuhusu suala la mahusiano. Waafrika wanaamini kuwa, mahusiano thabiti hujengwa katika misingi ya usawa wa kuheshimiana. Mwandishi anatufafanulia kwa kusema: “Usawa wa Kiafrika ni usawa wa kuheshimiana. Tangu zamani wazazi wetu waliheshimiana. Hii ni dhahiri kabisa. Ndiyo maana walikaa pamoja” (uk. 72). Kezilahabi anaendelea kupambanua misingi ya heshima kwa mujibu wa mtazamo wa Waafrika katika misingi ya ndoa ambapo kwa Waafrika, ni mwiko kwa mtoto wa kike kutaja jina la baba mkwe wake (uk. 6). Pia, anafafanua mahusiano ya ndoa baina ya mume na mke kama inavyotazamiwa na Waafrika. Hili linadhihirika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kupitia ukomo wa mahusiano ya Dennis na mkewe Vera ambaye aliishi katika kuikumbatia misingi ya Kizungu na kudharau asili yake ya Kiafrika. Mwandishi anatujulisha kwa kusema:

> Na ndani ya nyumba ya Dennis huo ndio ulikuwa mwisho wa jaribio la utamaduni wa “Kizungu”. Huo ndio ulikuwa mwisho wa jozi iliyojidai kuwa na mapenzi lakini kwa kutopeana heshima ikaanguka (uk. 110).

Katika nukuu hii, Kezilahabi anabainisha wazi kuwa Waafrika wana misingi yao ya kimaadili ambayo inabainisha mahusiano baina ya mume na mke. Hata hivyo, kufanya hivyo siyo kuzipinga tamaduni na mila za kigeni bali ni kuonesha kuwa kila jamii ina misingi na mipaka yake kitamaduni, ambayo imekitwa katika idili za jamii hiyo.

Kwa namna nyingine, Kezilahabi anawasilisha maudhui yake kuhusu falsafa ya Waafrika kwa kutumia dhana ya uduara. Katika kazi zake, anasawiri mtazamo kuwa Waafrika wameyakita maisha yao katika duara la maisha lisilo na mwisho. Mtazamo huu unasawiriwa katika falsafa ya maisha na kifo, kwamba; Waafrika wanaamini kuwa baada ya maisha ya mwanadamu hapa duniani, kuna mwendelezo wa maisha mengine katika ulimwengu wa wafu hai (Tempels, 1959; Mbiti, 2011 na Faustine, 2017). Katika riwaya ya *Nagona*, mtazamo huu umesawiriwa kupitia wanafalsafa wakongwe ambao wanakutanishwa na Mimi hata baada ya vifo vyao. Hii inadhihirika pale Babu anapomtambulisha Mimi kwa wanafalsafa hao kwa kusema:

> Uwaonao katika duara hii ni kikundi kidogo tu cha waliokuwa wabishi katika usakaji wa njia. Yule pale ni Plato na yule ni Socrates, huyu hapa ni Aristotle. Yule ni Hegel, huyu Darwin na waliokaribiana nawe ni Marx na Freud na huyu ni Nietzsche…Sasa hivi wametulia kidogo. Zamani wakianza majadiliano na roho zao ilikuwa vurugu tupu. Na wakianza majadiliano wao kwa wao basi hapa duara liliwaka moto (uk. 26).

Kutambulishwa kwa wanafalsafa hawa ambao walikwishakufa miaka mingi iliyopita, kunadhihirisha mtazamo mpana wa kifalsafa wa Waafrika kuwa maisha ni duara. Mwisho wa maisha ya mwanadamu hapa duniani ni mwendelezo wa maisha ya mwanadamu katika ulimwengu wa wafuhai.

### 4.2.3 Ujumi wa Mwafrika katika Mapambo

Suala la kuthamini mavazi na mapambo yanayoakisi utamaduni wa Mwafrika ni jambo jingine linalompambanua Kezilahabi kama mtetezi wa Uafrika. Hii inadhihirika kupitia kazi zake za fasihi pamoja na maisha yake halisi kama ambavyo tunafafanuliwa na watafitiwa uwandani. Katika kazi zake za fasihi, anaonesha mila na desturi za Waafrika kwa upande wa mavazi kupitia wahusika wake. Kwa mfano, katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, anabainisha uzuri wa mwanamke unaovuta matamanio ya mwanamume katika suala la mapenzi. Anarejelea mapambo ya ndani kama vile shanga ambazo huthaminiwa sana na mwanamke wa Kiafrika. Tunajulishwa hili kupitia masimulizi ya Leonila pale anaposema:

> Nilijikuta nimelazwa juu ya kitanda chake. Hapo ndipo aliponipa shilingi hamsini ili nivue nguo zote. Muda ulikuwa mfupi. Baada ya muda huu aliniomba nimvulie shanga zangu kumi za kiunoni kama zawadi na kama ahadi kwamba nitarudi siku nyingine, Tumaini aliniambia. “Siku utakayokuja tena uje umevaa shanga nyingi mpaka kitovuni…” (uk. 7).

Waafrika wanaamini kuwa shanga ni moja ya pambo ambalo humpendezesha mwanamke na pia ni chachu ya mapenzi. Hata hivyo, ameendelea kuonesha namna Waafrika wanavyolithamini pambo hilo kupitia mavazi ya kitamaduni wakati wa uchezaji ngoma kama inavyoelezwa katika nukuu ifuatayo:

> Ngoma iliyokuwa ikiitwa *abasenyeyi* ilikuwa na mlio mzuri sana. Wachezaji wote walikuwa wamevaa mavazi ya shanga pamoja na manyoya ya mbuni vichwani. Walichezesha mabega yao kwa utaratibu. Ukiwaangalia kwa nyuma utaona mabega yao yanakutana katikati na kutengana tena kama mbuzi wapiganao… (uk. 49)

Siyo katika kazi za fasihi peke yake, Kezilahabi alijipambanua pia kama Mwafrika halisi kwa namna alivyokuwa akiyaendesha maisha yake. Euphrase (*ktj*) anatueleza:

> Baba alipenda sana mavazi ya Kiafrika. Alipendelea sana kuvaa mashati ya vitenge. Mara nyingi alipokuwa akimletea mama zawadi, alimletea vitenge. Alikuwa ni mzuri sana kwenye kuchagua rangi zilizopangiliana vizuri.

Kwa Waafrika, kitenge ni vazi linaloheshimika na kuthaminika sana. Ndicho kitambulisho cha Mwafrika, mahususi nchini Tanzania kwa upande wa mavazi. Kezilahabi kupendelea mavazi hayo, ni dhahiri kuwa alilenga kusimamia misingi, tamaduni na mila za Kiafrika.

Kwa upande mwingine, Pantaleo (*ktj*) anafafanua mapenzi ya Kezilahabi katika kuuthamini ujumi wa Mwafrika kwa upande wa asili ya vitu. Anasema:

> Kihulka ni mtu aliyependa kuchunguza vitu vya asili. Mara nyingi alikusanya vitu mbalimbali vya kitamaduni kama vile vibuyu, vyungu, shanga, vigoda na kuvitumia. Pia, alipenda mapambo ya kiasili. Alikuwa akinunua vinyago mbalimbali vyenye asili ya makabila mbalimbali ya Afrika na mpaka leo viko nyumbani kwake.

Ubayana wa mapenzi ya Kezilahabi kwa vitu vya Kiafrika katika maisha yake halisi na hata namna anavyoakisi mitazamo ya Waafrika katika kazi zake za fasihi, ni uthibitisho tosha wa namna alivyojipambanua katika kuutetea Uafrika wake. Hii ni kwa sababu, kupitia maisha yake halisi na kazi zake za sanaa, watu hujifunza kuthamini na kuenzi utamaduni wa Waafrika na hatimaye kurithisha yale mazuri yenye tija kizazi hadi kizazi.

### 4.3 Tafiti za Kitaaluma

Katika mawanda ya kitaaluma, Kezilahabi amesimamia kuukuza na kuutetea Uafrika kupitia kazi zake mbalimbali. Hizi ni zile zinazojumuisha tafiti, uchapaji wa makala mbalimbali pamoja na utoaji wa taaluma zinazohusiana na maisha ya Waafrika kupitia mihadhara na mikutano mbalimbali. Tukianza na suala la tafiti, katika kusimamia misingi ya uelewekaji wa fasihi ya Kiafrika, alifanya utafiti katika shahada ya uzamivu mnamo mwaka 1985 akieleza umuhimu wa wahakiki na watafiti wa kazi za fasihi kuhakiki kazi zao kwa kuzingatia nadharia zenye misingi ya Kiafrika. Kezilahabi anafafanua kuwa kazi za Waafrika zitaeleweka kama tu zitahakikiwa na nadharia ambazo zimechipuzwa kutokana na fikra za Waafrika na kuakisi mazingira yao. Kezilahabi (2006), anasema:

> Hakuna nadharia ya uhakiki wa fasihi ambayo haijifungamanishi na mitazamo ya kifalsafa, na kwa hiyo, matumizi yoyote ya nadharia ya uhakiki pasipo uchambuzi wa kina unaojikita katika mtazamo wa kifalsafa yana upungufu. Uhakiki wa namna hii ni wa kidogma unaozalisha nadharia ambayo haileleweki vema. Pasipo kuzingatia mtazamo wa kifalsafa, mhakiki

> wa Fasihi ya Kiafrika atakuwa anavinjari ndani ya msitu wa masimulizi, tendi, riwaya, ushairi, na tamthiliya, zinazoonesha taswira, ishara na sitiari pasipo kuzielewa … ( imetafsiriwa na mwandishi wa makala)

Andiko hili la Kezilahabi limeibua ari na chachu kwa wahakiki na watafiti wa fasihi ya Kiswahili kufanya tafiti zao na kuhakiki kazi za fasihi za Kiafrika kwa kuzingatia misingi ya nadharia zinazokitwa katika falsafa ya Waafrika. Watafiti hao kwa kuwataja baadhi ni Chuachua (2016) ambaye amefanya utafiti wake kwa kuzingatia misingi ya Epistemolojia ya Wabantu. Pia, Faustine (2017) amefanya utafiti wake kwa kujikita katika Nadharia ya Uhalisiajabu ambayo inafungamana na misingi ya falsafa ya Kiafrika.

Pia, alitafiti ngoma mbalimbali za Kiafrika akiwa nchini Botswana. Mfano ni ngoma ya Waswarwa ambayo alikusanya nyimbo zake, kurekodi na kuwa anasikiliza huku akitafiti ujumbe na dhima za ngoma hizo katika jamii. Euphrase (*ktj*) anatuambia:

> Baba alipenda sana ngoma za asili. Akiwa Botswana alipenda kutembelea vijiji mbalimbali. Huko alitafiti na kurekodi ngoma za Waswarwa. Alipenda kusoma *dance* zao na kuelezea mitazamo ya maisha wanayoishi. Alipenda kusema ngoma zina ujumbe mkubwa unaohusiana na jamii husika.

Kezilahabi anapambanua ujumi wa ngoma kwa kadiri ya mtazamo wa Waafrika katika kazi zake za fasihi. Katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, anasema: “ngoma ni chakula cha Mwafrika” (uk. 50). Kimsingi, nukuu hii inadhihirisha thamani ya ngoma kwa Waafrika. Hii ni kwa sababu kupitia ngoma hizo, jamii mbalimbali ulimwenguni huweza kujifunza mambo mbalimbali ambayo ni pamoja na utamaduni na pia kubaini fahari ya Waafrika,

Licha ya kutafiti ngoma za makabila mbalimbali, Kezilahabi alishiriki pia kuimba nyimbo za kabila lake la Kikerewe na kupiga zeze (*Enanga*). Euphrase (ktj) anafafanua hivi:

> Kuna siku alitupigia *Enanga* (zeze) na watoto wenzangu. Tulikuwa tuna kawaida ya kukutana kila Jumamosi na familia za wafanyakazi wenzake kama Profesa Amandina Lihamba, Profesa Penina Mlama, na mama Masanja. Katika mkusanyiko huo tulifunzwa nyimbo za Kiswahili, michezo ya watoto, pamoja na hadithi. Jukumu kubwa la baba katika mkusanyiko huo ni kupiga *Enanga*.

Kimsingi, kama mtu hathamini fahari ya utamaduni wake na kujua thamani ya fahari hiyo hawezi kushiriki katika utendaji wake. Kezilahabi aliitambua fahari na thamani ya tamaduni za jadi yake katika kuelimisha, kuadilisha na kuiburudisha jamii ndio maana alikuwa tayari kushiriki moja kwa moja katika matukio mbalimbali yaliyohusisha jadi za Kiafrika.

Pia, Kezilahabi alihudhuria katika makongamano na mikutano mbalimbali ambako aliwasilisha mada zilizolenga kuikuza na kuiendeleza fasihi ya Kiafrika.

Miongoni mwa mikutano aliyohudhuria ni ule wa waandishi wa fasihi ya Kiafrika. Katika mkutano huo, alibainisha lugha inayofaa kutumika katika uandishi au uwasilishwaji wa fasihi ya Kiafrika kuwa ni ile inayoeleweka kwa Waafrika wenyewe. Jambo hili linajipambanua zaidi katika Kezilahabi (2012:106) anaposema:

> Fasihi inashughulika na utambuzi kuhusu sisi ni akina nani "utu wetu" (u - sisi) na inatuonesha katika unia nzima kiasi kwamba dunia iweze kutufahamu tulivyo. Katika fasihi, sio tu kwamba tunajieleza wenyewe bali tunajitambulisha pia. Ni mtazamo wangu kuwa lugha nzuri ya kutumiwa ni ile iliyo karibu yetu kiontolojia. Hii inamaanisha kuwa fasihi ni kitu cha kwanza na cha kipekee kiontolojia ambacho kupitia kwacho, wanadamu wanaonekana kukifungamanisha na jamii na mahusiano ya kijamii kwa kadri wanavyoitengeneza historia yao (imetafsiriwa na mwandishi wa makala).

Nukuu hiyo inafafanua wazi mtazamo wa Kezilahabi kuhusu lugha inayopaswa kutumiwa katika kazi za fasihi. Anaweka bayana kuwa fasihi ni chombo ambacho kinabainisha utu wetu kama tulivyo pamoja na mahusiano ya kijamii. Ni chombo ambacho kinatengeneza historia yetu katika nyakati tofauti. Siyo tu kwamba fasihi inatuwezesha kujieleza na kutoa hisia zetu, bali pia inatuwakilisha mahali pengi duniani kwa namna tulivyo. Ni katika muktadha huu ambapo anatetea fasihi ya Waafrika kuwa lugha mwafaka ya kutumiwa katika fasihi yao, ni lugha asilia zinazoakisi kuwapo kwao.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha namna Kezilahabi alivyojipambanua katika kuutetea Uafrika. Makala imethibitisha kuwa Kezilahabi ni nguli wa fasihi ya Kiafrika aliyeutetea Uafrika wake kupitia kazi za fasihi kwa namna anavyoifinyanga fani na maudhui yenye kuakisi mazingira, mila na desturi za Waafrika. Hii ni pamoja na matumizi ya lugha ya Kiswahili kama nyenzo muhimu ya kuwasilisha maudhui mbalimbali katika kazi za fasihi. Jambo hili linaifanya fasihi kuwa na asili yenye kuibeba taswira nzima ya Waafrika. Aidha, anajipambanua pia kupitia maisha yake halisi ndani na nje ya taaluma yake kwa kushiriki katika tafiti, midahalo na makongamano mbalimbali ambapo alifanya tafiti, na kuwasilisha makala mbalimbali zilizohusiana na maisha ya Waafrika na uandishi wa kazi zao.

## Marejeleo

Bitende, F. (2012). *Taswira za Kidini katika Riwaya za E. Kezilahabi*. Tasinifu ya Digrii ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Chalmers, F.G. (1973). "The Study of Art in a Cultural Context". *The Journal of Aesthetics and Art Criticism,* 32(2): 249 - 256.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Faustine, S. (2017). *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Gaudioso, R. (2020). "To the Eternal Presence of Poetry, to Euphrase Kezilahabi". *Swahili Forum*, 27:5-16.

Kezilahabi, E. (1988). *Karibu Ndani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (2003a). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111, Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI (145 – 165).

Kezilahabi, E. (2003b). "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111, Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI (226 – 243).

Kezilahabi, E. (2006). *African Literature and the Problem of Literary Criticism.* Published Ph.D. Thesis, University of Wisconsin, Madison.

Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja wa Fujo*: Nairobi. Vide-Muwa Publishers Limited.

Kezilahabi, E. (2012). "Erasure and the Centrality of Literatures in African Languages". *Kiswahili,* 75:104 – 117.

Khamis, S. A. M. (2007a). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, 5: 13-23.

Mbatiah, M. (1998). "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*". *Mulika*, 24: 1-11.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religion and Phylosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (1983). "*Dunia Uwanja wa Fujo* (Mapitio ya Kitabu)". *Kiswahili*, 50(1): 1-12.

Musau, P. M. (1985). *Euphrase Kezilahabi: Mwandishi Aliyekata Tamaa*.Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Nairobi.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Senkoro, F. E. M. K. (1995). "Euphrase Kezilahabi Shaaban Robert wa Pili". *Kioo cha Lugha*, 1(1): 61- 69.

______(2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano ya Fasihi Andishi na Simulizi" *Kioo cha Lugha*, 4: 22-38.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy.* Paris: Presence Africaine.

Wellek, R. (1959). Hippolyte Taine's Literary Theory and Criticism. *Criticism*, (1):1-18. Imesomwa tarehe 11/03/2021 katika http://www.jstor.org/stable.